

UKWELI UNAPASHWA KUJUWALI.

KUVA A MASKI



NI SALAMA ZAIDI KUVA A MASKI

COVID-19 bado inaambukiza maelfu ya watu kila siku wakiwemo wazee, watu wazima, vijana na watoto. **Bila kujali kama maski zinahitajika katika eneo lako, wewe na familia yako mtakuwa salama zaidi ikiwa mtavaa maski.**

Maski hulinda dhidi ya

COVID-19

Kwa sababu COVID-19 huenea kwa urahisi sana, kuvaa maski hukulinda wewe, marafiki na familia yako, na jamii yako.

- ✓ Unapovaa maski, kuna uwezekano mdogo kwamba utaogua kutokana na kupumua virusi ndani ikiwa viko hewani.
- ✓ Inawezekana uwe mgonjwa kutokana na COVID-19 na usijue, kwa sababu sio kila mtu anahisi kuwa mgonjwa. Katika hali hii, kuvaa maski hufanya kuwe na uwezekano mdogo kwamba utaeneza virusi kwa wengine.



MASKI LAZIMA ZIVALIWA VIZURI ILI KUWA NA UFANISI.

- Vaa maski yako ukiwa umefunika pua na mdomo wako
- Hakikisha hakuna hewa inayovuja katika sehemu ya juu au pande
- Vaa na uvue maski yako ukitumia mikono safi
- Usiguse maski yako ikiwa kwenye uso wako
- Safisha maski yako inayoweza kutumika tena angalau kila siku
- Tumia maski yako isiyoweza kutumika tena, mara moja tu



Chanjo hutoa ulinzi zaidi

- Kupata chanjo ni hatua muhimu zaidi kwako kuchukua ili kujilinda wewe na jamii yako.
- Baada ya kupata chanjo kamili kuna uwezekano kwamba utaogua kutokana na COVID-19, na hata ukiogua, chanjo hiyo itakulinda dhidi ya kupata ugonjwa hatari.

HATA WATU WALIOPEWA CHANJO NI SALAMA ZAIDI WAKIWA NA MASKI

Sio kawaida kwa watu kuogua COVID-19 baada ya kuchanjwa, lakini inaweza kutokea.

Kupata chanjo na kuvaa maski ni njia bora zaidi za kuepuka kuogua na kueneza COVID-19 kwa wengine.